



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**



**OKTOBA 12,2023.**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **BEI ELEKEZI YA MBOLEA ZA RUZUKU HALMASHAURI YA MJI NJOMBE KWA MSIMU WA KILIMO 2023/2024 KWA KILA KATA.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwataarifu wakulima wote kuwa ; katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 serikali imeendelea kutoa zuruku katika mbolea mbalimbali kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija katika Kilimo na hatimaye kuwa na uhakika wa chakula na kuongeza pato la mkulima.

Katika kutekeleza hilo Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) imeboresha mfumo wa usambazaji wa mbolea kwa kuweka bei elekezi kwa kila kata kwa aina zote za mbolea zenye ruzuku katika ujazo wa kilo 50 na kilo 25.

Aidha mawakala wote walioidhinishwa kuuza mbolea za ruzuku kwa wakulima mnakumbushwa kuepuka udanganyifu kwa kuzingatia bei iliyopangwa na serikali.

Bei pamoja na vituo vya kuuzia mbolea kwa kila kata zinapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ambayo ni **[www.njombetc.go.tz](http://www.njombetc.go.tz)**

Halmashauri ya Mji Njombe inawatakiwa wakulima wote mafanikio kwenye msimu huu wa kilimo wa 2023/2024.

**Imetolewa na:**

**Ichikael Malisa**

**Afisa Habari**

**Halmashauri ya Mji Njombe.**